**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**

SHULE YA SEKONDARI LUMUMA,
S.L.P. 280,
**KILOSA.**
**11/12/2020**

**KUMB. Na. LUM/S.2200/FI – 2021/JI**

JINA LA MWANAFUNZI ........................................................
S.L.P. ..................................
..............................................

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUMUMA KWA MWAKA WA MASOMO 2021.</u>**

1: **UTANGULIZI:**

Ninafuraha kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) katika shule hii mwaka 2021. **Shule ya sekondari Lumuma inakupongeza na kukukaribisha sana.**

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021, unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 22/01/2021.

2: **MAHALI SHULE ILIPO:**

Shule hii ipo katika kijiji cha **Idole-Lumuma** ambapo ndio makao makuu ya Kata ya Lumuma pembezoni mwa barabara iendayo Kilosa kutoka kwenye ofisi za Kata Lumuma

3: **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

**A: SARE YA SHULE**

(i) **WASICHANA**

- Sketi mbili (2) mshono linda box ndefu kupita kwenye magoti zisizobana; rangi DAMU YA MZEE
- Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi **<u>aina ya TOMATO</u>** yasiyobana.
- Soksi nyeupe
- Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba na visivyo na visigino virefu.
- Hijabu ndefu na nusu kanzu kwa wanafunzi wa kike wa kiislam.

(ii) **WAVULANA**

- Mashati mawili meupe mikono mifupi **<u>aina ya TOMATO</u>** yasiyobana.
- Suruali mbili ya rangi ya DAMU YA MZEE yenye malinda mawili kila upande zisizobana
- Viatu vyeusi vya ngozi visivyochongoka vya KAMBA (KUMBUKA!! SIYO RABA NYEUSI).
- Soksi nyeusi
- Mkanda mweusi wenye kichuma cha kawaida cha kufungia.

Scanned with CamScanner

**B: VIFAA VYA DARASANI**

- Madaftari makubwa (Counter book Q2 au 3) 10
- Mkebe wa Hesabu (Mathematical set)
- Kalamu za wino (blue or black) za kutosha
- Rula, kalamu za risasi, graph pad, n.k.
- Kamusi ya Kiingereza
- Vitabu vya masomo mbalimbali yanayofundishwa hapa shuleni
- Begi la kubebea vifaa vyake **(KUMBUKA: SIYO MFUKO)**

**C: SARE ZA MICHEZO**

- T-Shirt aina ya form Six rangi ya Dark blue kwa wasichana na wavulana (NI LAZIMA).
- Bukta ya blue kwa wavulana
- Tracksut ya blue kwa wasichana

**D: VIFAA VYA USAFI SHULENI**

- Jembe moja (1) jipya lenye mpini wake
- Fyekeo au Reki moja
- Ndoo ndogo moja (ujazo lita kumi)
- Ufagio wa chelewa mmoja

**E: MAZINGIRA**

- Aje na mche wa mti wa matunda ambao ataupanda na **ATAUHUDUMIA MWENYEWE.**

**KUMBUKA!!**

(i) Si vyema kumnunulia mwanafunzi sare ya mwanafunzi aliyemaliza.

(ii) UKAGUZI WA VIFAA NA SARE UTAFANYIKA SIKU MWANAFUNZI ANAPORIPOTI

(iii) MWANAFUNZI ATAPOKELEWA ENDAPO TU ATAFUATA TARATIBU NA MAELEKEZO YOTE YA KUJIUNGA NA SHULE.

**F: CHAKULA CHA MCHANA CHA WANAFUNZI**

CHAKULA CHA MCHANA KWA WANAFUNZI WOTE KINATOLEWA HIVYO KILA MZAZI/MLEZI ASHIRIKI KUHAKIKISHA KUWA WANAFUNZI WANAPATA CHAKULA HICHO KWA KUKAMILISHA MICHANGO TULIYOKUBALIANA KWA WAKATI.

(i) Lita 25 za chenga za mahindi kwa nusu muhula (Januari – Juni)

(ii) Lita 10 za maharagwe kwa nusu muhula (Januari – Juni)

**4: ULINZI WA MALI ZA SHULE NA BINAFSI**

Kila mwanafunzi lazima awe mlinzi na mtunzaji wa mali zote za shule, zake binafsi na za wenzake.

**5: MWISHO**

Nachukua nafasi hii kukukaribisha katika shule ya sekondari Lumuma na nimatarajio ya shule kuwa utaitumia vyema nafasi hii uliyopewa na Taifa lako.

..............................

**MKUU WA SHULE**

Scanned with CamScanner

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**

**SHULE YA SEKONDARI LUMUMA**

# SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Pia inazingatia miongozo/maelekezo yote yanayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

**Hivyo:**

(i) **MAHUDHURIO:**
Mwanafunzi hana budi kuhudhuria vipindi vyote vya masomo Darasani na nje ya darasa kama ilivyoelekezwa na Mamlaka husika; (yaani siku 192 kwa mwaka).

(ii) Mwanafunzi hana budi kuwaheshimu au kuwatii watu wote; walimu, wafanyakazi wasio walimu, viongozi na wageni wanaofika shuleni.

(iii) Mwanafunzi aepuke vitendo viovu kama: matusi, utoro, wizi, ugomvi, ulevi / pombe, madawa ya kulevya, uvutaji sigara/bangi, uasherati, ushoga, kuoa au kuolewa, kuchochea migomo, n.k.

(iv) Mwanafunzi hapaswi kuvaa vidani kama vile; herein, mikufu, bangili.

(v) Mwanafunzi hapaswi kutia dawa nywele au kujichora tattoo sehemu za mwili wake.

(vi) Kusimama wakubwa wanapopita karibu yako na kuwasalimu ndani na nje ya darasa.

(vii) Mwanafunzi hatakiwi kutembelea nyumba za kulala wageni na kumbi za starehe.

(viii) Mwanafunzi hapaswi kuwa na kucha ndefu na kutopakaa rangi au hina kucha zake.

(ix) Wavulana hawaruhusiwi kufuga ndevu wala kuwa na nywele ndefu.

(x) Wasichana Hawaruhusiwi kuwa na nywele ndefu (nusu inchi)

(xi) Mwanafunzi ni lazima kuvaa SARE ya shule muda wote wa masomo darasani na nje ya shule kwa shughuli za kishule tu.

(xii) Mwanafunzi hapaswi kuwa na simu ya mkononi, sim CARD au vocha awapo shuleni.

(xiii) Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia, jaketi, sweta ambalo siyo la shule.

(xiv) Mwanafunzi anapaswa kufanya usafi binafsi na wa shule kwa ujumla.

(xv) Mwanafunzi anapaswa kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote.

(xvi) Ni lazima aheshimu Bendera na Wimbo wa Taifa.

(xvii) Hatakiwi kuandika katika vitabu vya shule, kuta, madawati, viti, meza na mbao za kufundishia.

(xviii) Kutofanya biashara ya aina yeyote katika eneo la shule.

Scanned with CamScanner

**HATUA ZICHUKULIWAZO KWA KUKIUKA TARATIBU, KANUNI NA SHERIA ZA SHULE**

- Kuonywa
- Kufanya kazi za mikono za ziada
- Kupigwa viboko
- Kusimamishwa shule

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA MWANAFUNNZI KUFUKUZWA SHULE**

(i) Wizi
(ii) Uasherati
(iii) Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya
(iv) Uvutaji sigara/bangi
(v) Makosa ya Jinai
(vi) Kupigana au kupiga
(vii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
(viii) Kudharau Wimbo na Bendera ya Taifa
(ix) Kuoa au kuolewa
(x) Kuwa na mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
(xi) Kugoma, kuchochea na kuongeza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa shule na watu.
(xii) Kukataa adhabu HALALI kwa makusudi

..................................
**MKUU WA SHULE**

Scanned with CamScanner

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**

**SHULE YA SEKONDARI LUMUMA**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ULIYOPEWA**

Bandika picha hapa

(Passport yenye shati jeupe)

**A: TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

- Jina kamili la mwanafunzi ……………………………………………………………………
- Tarehe ya kuzaliwa: ……………………………….(ambatanisha nakala ya cheti cha kuzaliwa)
- Mahali ulipozaliwa ………………………………………………………………………………
- Uraia ………………………………………………………………………………………………
- Shule uliyotoka: ………………………………………………………………………………..
- Namba ya mtihani: Ps …………………………………………………………………………

**B: TAARIFA YA MZAZI/MLEZI**

- Jina la Mzazi/Mlezi: ……………………………………………………………………………
- Kazi ya Mzazi/Mlezi: ……………………………………………………………………………
- Anuani ya mzazi/mlezi: …………………………………………………………………………
- Namba ya simu ya mzazi/mlezi: ………………………………………………………………

**C: MWANAFUNZI**

Mimi ……………………………………………………..nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote kwa hiyo nakubali kuipokea afasi niliyopewa. Ninaahidi kufuata sheria na taratibu za shule na kujifunza kwa bidii.

Saini: …………………………………… Tarehe: ……………………………..

**D: MZAZI/MLEZI**

Mimi ……………………………………………………………… Nimehakikisha mwanangu amezisoma na kuzielewa sheria na taratibu za shule na nimemsisitiza katika hilo. Pia naahidi kutokuwa kikwazo kwa mwanangu katika kujipatia Elimu yake.

Saini: …………………………………… Tarehe: ……………………………..

***KUMBUKA: Fomu hii ijazwe kwa umakini na irudishwe shuleni mwanafunzi anaporipoti.***

Scanned with CamScanner

**THE PRESIDENT'S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**
**KILOSA DISTRICT COUNCIL**

LUMUMA SECONDARY SCHOOL,
P.O.Box 280,
**KILOSA.**

**REF. No. USS/REG/VOL.1/..........** ..................

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

FROM: THE MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL
......................................
......................................

TO: THE HEAD OF SCHOOL,
LUMUMA SECONDARY SCHOOL,
P.O.Box 280,
**KILOSA.**

**RE: MEDICAL CERTIFICATE FORM.**

I have examined ....................................................................... who aspires to join form one in your school as follows:-

| No | AREA | REMARKS |
|---|---|---|
| 1 | Skin | |
| 2 | Eyes | |
| 3 | Ears | |
| 4 | Teeth | |
| 5 | Chest | |
| 6 | Spleen | |
| 7 | Abdomen | |
| 8 | Urine | |
| 9 | Stool | |
| 10 | HB Hemoglobin | |
| 11 | In a collation against meningitis | |
| 12 | Sickle cells | |
| 13 | Asthma | |
| 14 | Pregnancy (If applicable) | |

ADDITION INFORMATION:- Eg. Physical defects or impairments, infection, chronic or family diseases etc.
.........................................................................................................
.........................................................................................................
.........................................................................................................

I certify that the above is physical fit/unfit for admission
Signature .................................................
Destination ..............................................
Station ......................................................
Date .........................................................
Official Stamp ..........................................

Scanned with CamScanner